**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**Simu:Na.+255 22 211 3165**

**Nukshi Na: +255 22 212 4576**
**Barua pepe:cl@ardhi.go.tz**

**1 MTAA WA ARDHI**
**S. L. P 9230**
**11477, DAR ES SALAAM.**

**Tafadhali unapojibu taja:**

**Kumb.Na.LD/350196/158**

**14/01/2022**

Mkurugenzi Mtendaji,
Selfina East Africa Limited,
S.L.P 31310,
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: KUTENGEWA ARDHI KIASI CHA EKARI 50 KWA AJILI YA UWEKEZAJI KATIKA ENEO SOGA WILAYA YA KIBAHA MKOA WA PWANI.**

Husika na kichwa cha habari hapo juu na urejee barua yako isiyo na kumbukumbu namba wala tarehe.

2. Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Pwani, inakiri kupokea barua yako yenye kichwa cha habari hapo juu, uliyomuandikia Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ukiomba ardhi kwa lengo la uwekezaji katika Wilaya ya Kibaha.

3. Tunachukua fursa hii kukujulisha kuwa kwa kuzingatia ardhi iliyopo umetengewa ekari 50 katika eneo la Soga kwa ajili ya kukuwezesha kutekeleza mradi wako.

4. Aidha ili kutuwezesha kuendelea na hatua zaidi unaombwa kutuwasilishia nyaraka muhimu kama ifuatavyo:

i. Taarifa ya sasa (Current) ya upekuzi wa kampuni (Search) toka Brella.
vi. Ni muhimu pia kutufahamisha kama umesajiliwa na taasisi za uwekezaji nchini kama vile TIC au EPZA ukiambatisha na udhibitisho wa usajili huo.

Tunategemea ushirikiano wako.

Bishanga, T.H
**KNY: KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI**
**MKOA WA PWANI**

Nakala: Katibu wa Mkuu wa Mkoa,
Mkuu wa Mkoa wa Pwani,
S.L.P. 30080,
**KIBAHA-PWANI.**